REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF LAIKIPIA

THE HANSARD

Wednesday, 15th May, 2024

The House met at the Assembly Chambers at 10.00 a.m.

[The Speaker (Hon. Lantano Nabaala) in the Chair]

PRAYERS

QUORUM CALL

Speaker: Clerk, confirm whether we have got quorum.

(Lack of quorum confirmed)

Speaker: I direct that the bell be rang for ten minutes.

(The quorum bell was rung for 5 minutes)

Hon. Mary Gathoni: Mr. Speaker, we have got quorum.

Speaker: Clerk, confirm whether we have got quorum.

(Lack of quorum confirmed)

Speaker: The bell may continue ringing.

Hon. Stephen Ndiritu: Mr. Speaker, I can see that we are full House.

Speaker: Clerk, confirm to that effect.

(Clerk confirmed achievement of Quorum)

Speaker: Now that we have got quorum, we will proceed with the business of the House.

COMMUNICATION FROM THE CHAIR

INFORMAL MEMBERS MEETING

Speaker: Thank you, Hon. Members. I want to bring to your attention information pursuant to our calendar of the Assembly that in due time, in about a week we will be proceeding for our recess. Hon. Members, it is good for us to plan things as a House. So, I want to relay to you that we need to have all Members *kamukunji* after this first session within the chambers. Thank you.

NOTICES OF MOTIONS

PROVISION OF FLOOD VICTIMS IN THE COUNTY WITH BASIC NECESSITIES

Hon. Catherine Umija: Thank you, Mr. Speaker. I beg to give notice of the following motion;

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

THAT, AWARE THAT, pursuant to article 43 (1c) of the Constitution of Kenya 2010, every person has the right to be free from hunger and to have adequate food of acceptable quality;

FURTHER AWARE THAT, The Laikipia County Disaster Risk Management Act, 2019 defines disaster as progressive or a sudden, widespread or localized, natural or human-caused occurrence affecting the functioning of an entire or a section of community which-

a) causes or threatens to cause- death, injury or disease; damage to property, infrastructure or the environment; or disruption of the life of a community; and

b) is of magnitude that exceeds the ability of the community affected by the disaster to cope with its effects using only its own resources;

CONSCIOUS OF THE FACT THAT, the Country has been experiencing heavy downpour rainfall which has caused floods in various parts of the country, leading to destruction of properties and loss of lives;

CONCERNED by the huge damage of farm crops and displacement of people by floods in Laikipia County;

ALARMED by the status of the camping sites where the displaced persons have inadequate food stuffs, blankets and shelter;

APPRECIATING THAT, section 10(2) of the Contingencies Fund and County Emergency Fund Act, 2011 stipulates that, the purpose of the emergency fund is to enable payments to be made in respect of a County when an urgent and unforeseen need for expenditure arises for which there is no specific legislative authority; this House URGES the County government to assist the flood victims with food, blankets and shelter.

REPORT ON STATUS OF STREET AND FLOOD LIGHTS IN THE COUNTY

Hon. Caroline Kihika: Mr. Speaker, I beg to give notice of the following motion;

THAT this Assembly adopts the report on street lighting and flood lights status at various wards across the county by the County Cohesion Justice and Legal Matters Committee dated 13th February, 2024.

UNCLOGGING OF DRAINAGE SYSTEMS IN URBAN AREAS

Hon. Caroline Kihika: Mr. Speaker, I beg to give notice of the following motion;

THAT AWARE THAT Part 2 of the Fourth Schedule of the Constitution of Kenya 2010, stipulates that County public works and services, including storm water management systems in built-up areas is a function of the County Government;

NOTING THAT the Country has been experiencing enhanced rains since April, 2024 with alarming levels of rainfall because of El Nino conditions;

CONCERNED THAT El Niño rains have caused widespread and extensive flooding which destroyed property in the County occasioned due to blocked drainage systems in urban centers;

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

This House URGES the County government to clear drainages during the rainy season to avert artificial flooding of the urban areas and to build and maintain proper drainage systems and culverts to divert excess water.

PROVISION OF WAIVER ON LAND RATES ACCUMULATED INTEREST AND PENALTIES

Hon. Stephen Ndiritu: Mr. Speaker, I beg to give notice of the following motion;

NOTING THAT Section 159 of the Public Finance Management Act, 2012 empowers the County Executive Committee member for finance with the approval of County Assembly to waive county tax, fee or charge imposed by the County Government and its entities;

FURTHER NOTING THAT most of the Land Owners are hesitant to pay for land rates because of the accumulated interest and penalties due to adverse external factors including a depressed economy, prolonged drought and subsequent floods which have affected citizens' ability to pay which amounts to Kshs. 922,817,891;

This House URGES the County Government pursuant to the provisions of Section 159 of Public Finance Management Act, 2012 to provide 100% waiver on accrued penalties and interests on land rates for a period of one month with effect from 17th May, 2024 to 17th June, 2024 to offer much-needed relief to rate payers.

ASSESSMENT OF LOSSES AND PROVISION OF SEEDS TO FLOOD AFFECTED FARMERS

Hon. Salim Edung: Thank you, Mr. Speaker. I beg to give notice of the following motion;

THAT AWARE THAT Part 2 of the Fourth Schedule of the Constitution of Kenya 2010, stipulates that Agriculture, including crop and animal husbandry is a function of the County Government;

FURTHER AWARE THAT firefighting services and disaster management is a function of the County Government;

CONCERNED of the ongoing heavy rains experienced in the Country which has damaged crops by washing away seeds, seedlings and mature plants leading to significant losses to farmers; this House URGES the County Government to undertake an assessment of the losses caused by the floods and supply available seeds to flood-affected farmers so they can plant and regain a harvest as flood waters recede.

MOTIONS

ASSESS AND REPAIR ROADS DAMAGED BY FLOODING FROM EL-NINO RAINS

Hon. Stephen Ndiritu: Thank you, Mr. Speaker. I beg to move the following motion;

THAT, Aware that Part 2 of the Fourth Schedule of the Constitution of Kenya 2010, stipulates that County transport, including county roads is a function of the County Government;

NOTING THAT the Country has been experiencing enhanced rains since April, 2024 with alarming levels of rainfall because of El Nino conditions;

CONCERNED that El Niño rains can have had significant impacts on roads and infrastructure in the County; Further Concerned that the heavy rainfall has led to

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

erosion, flooding, damaging roads, bridges and other infrastructure which has resulted to road closures, travel disruptions and increased maintenance costs for repairs;

this House URGES the County Government to assess the extent of the damage occasioned by the floods, to determine the scope of the repairs needed and prioritize repairs based on the severity of the damage and the importance of the road in the transportation network.

Bwana Spika, huu ni mswada ambao unazungumzia kuhusu barabara zetu ambazo tunapitia na ziko chini ya Serikali ya Kaunti. Kuna Barabara ambazo ni za Serikali Kuu na zile za serikali ya ugatuzi na barabara ambazo nazungumzia hapa ni zile za serikali ya ugatuzi, ikizingatiwa ya kwamba serikali ya ugatuzi ndiyo iko na jukumu ya kuhakikisha barabara za *feeder roads* na barabara kuu, zingine zinafaa kuangaliwa kila wakati na kufanyiwa marekebisho.

Kwa sasa, ningetaka kufahamisha Wabunge kama vile wanavyoelewa ya kwamba kulikuwa na mvua ya El-nino ambayo imeweza kunyesha katika Taifa letu la Kenya na Laikipia haikuepuka hiyo mvua. Ndio maana nimeleta huu mswada ndio serikali kupitia wahandisi ambao wameajiriwa kwa pesa ya umma na pia Idara ya Ujenzi na Barabara waweze kuingia katika hizo barabara, kuziangalia na kuhakikisha ya kwamba zile ambazo zimeharibika tumeambiwa ni kiwango kipi.

Hii mvua, kuna sehemu ambazo ilinyesha zaidi kama sehemu za Ngobit, Marmanet, Sosian, Tigithi na sehemu zote kuanzia Umande hadi Laikipia Magharibi na pia Laikipia Mashariki. Hata ukiangalia kwa mitandao, sio Laikipia pekee lakini kuna sehemu zingine ambapo wananchi wamebebwa na maji. Tuliona lori ambayo ilifyekwa na maji ikiwa imebeba wananchi. Kwa hivyo, hiyo mvua ilikuwa ikipita kwa Barabara ikiwa inaharibu culverts na pia kukata Barabara. Ni jukumu la serikali kutembea wadi zote na kukagua kiwango ambacho kimeharibiwa na mvua hii.

Bwana Spika, kwa mfano, mahali nimetoka kuna barabara ambayo imetoka *Blue Gum* kuelekea Baraka na imekatika mara mbili. Hata *culverts* zimekatwa. Kwa hivyo, ni vizuri wahandisi waweze kufika pale kuiangalia na pia kuitengeneza. Hofu ambayo niliyo nayo ni ya wale wakandarasi ambao wamepewa kazi katika Laikipia. Wengine wakati tunapoongea hapa, Barabara ambazo zilitengenezwa na huyo mtu hajapewa cheti wala kufanyiwa ukaguzi, zingine zimesobwa na maji.

Ndio maana nataka serikali iamke haraka ili iweze kuangalia na kujua wale wakandarasi ambao walikuwa wamepatiwa kazi na kumaliza lakini idara ikazembea na kukosa kufanya ukaguzi kabla ya mvua kunyesha na kusomba Barabara hizo. Wajue vile watagharamia pamoja na wale wakandarasi kwa sababu itakuwa sio jambo la busara ya kwamba kuna mamilioni ya pesa hapo, serikali wako pale na hawaendi kukagua halafu mvua ikija inakata. Hii mvua ilinyesha hadi lami zikakatwa. Sasa mimi najiuliza, zile Barabara ambazo ziko huko mashinani, ziko katika hali gani?

Ukienda hapa Majengo na ni mjini, barabara imekatika. Ukienda sehemu zingine kama Ngobit, barabara imekatwa katikati kama kilomita tatu na hiyo barabara ilikuwa nzuri. Nasema hivyo ili Mheshimiwa Kihika asiende kwa sababu yeye anaelewa haya mambo ya ujenzi na pia yeye ndiye atakayeafiki wa huu mswada. Kwa hivyo, itakuwa ni jambo la busara kama tutaelewa ni nini tutakachofanya. Naomba serikali kupitia kwa Waziri Nabos na Mhandisi Macharia waweze kuingia katika Barabara zetu na wapate kujua zimeharibika kwa kiwango kipi.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

Bwana Spika, kuna pesa ambazo huwekwa za dharura na kisheria lazima ziwe pale lakini hatujui hizi pesa huwa zinapelekwa wapi. Kwa wakati ndio tunafaa kuona hizo pesa zikifanya kazi. Sheria husema 2% ya bilioni saba zinafaa kuwa pale lakini mwishowe hatujui huwa zinaenda wapi? Ama ni Msalaba Nyekundu ipi ambayo iko ndani ya serikali ambayo huwa ikibeba pesa zote na kwa hivyo, ni lazima tuwe macho. Hizo pesa zote tunataka zichukuliwe zitengeneze zile Barabara ambazo zimeharibika na pia zile *culverts* ambazo zimekatika ziongezewe kwa sababu ninajua ya kwamba ni pesa nyingi na huwa tunapitishia bajeti hapa.

Bwana Spika, kwa sababu tuko na biashara zingine ambazo tunapitisha, bila kuzungumza mengi, hawa wabunge wanajua mahali ambapo wametoka. Sioni mtu ambaye anaweza kujidai ya kwamba yeye hukaa kwa ghorofa na hushuka kwa lami na kuingia kwa Bunge. Hata kama yuko, lazima awe na nyanya mahali ambapo huwa anatembea kama Umande, Ngobit au Mukogodo huko mashinani.

Kama upande wa Magharibi Bwana Spika, unajua huko ni kubaya kwa sababu Barabara za huko zimekatwa. Huko Barabara ni mchanga na maji huwa ikipita na huo mchanga. Ni vizuri tuungane ili tuambie serikali ya kwamba huu ni wakati wa kuangalia pesa za dharura ili zichukuliwe mara moja. Tuambie serikali ya kwamba huu ni wakati wa kuchukua pesa za dharura kwa maana hizo huwa hazihitaji mikakati mingi. Kwa hayo machache, naomba Mheshimiwa Caroline Kihika kutoka Marmanet na anajua vile mvua ilinyesha huko, aweze kuunga huu mswada mkono. Asante.

Hon. Caroline Kihika: Thank you, I rise to second the motion. I am very grateful that our member of the Assembly has noticed that. It has been a concern to everybody because there was a nature calamity. The county has got disaster money and therefore, it is upon the House to join hands and have the nature and destruction analysed and this be done with speed since some of these roads that have been destroyed. We have kids passing by them on their way to school and they are using longer routes to get to school. Patients need to be taken to the hospitals and roads are impassible. So, I beg the House to join hands and let the disaster money be used to repair roads.

(Question proposed)

Hon. Anthony Theuri: Asante sana, Bwana Spika. Nasimama kuunga huu mswada mkono. Kama vile Mjumbe mwenzangu amesema, mvua imeleta madhara mengi sana. Hakuna mahali ambapo hii mvua haijaguza. Mimi binafsi, siku ambazo zimepita, maji yamekuja kwa njia kubwa na kubeba nyumba na kuleta hasara nyingi sana. Hivi karibuni, natoa tahadhari na taarifa ya kwamba mambo katika hili Bunge yatabadilika kwa sababu tutaanza kuleta taarifa baada ya taarifa na tutakalisha watu katika viti za miiba na hatutacheka nao tena. Sisi tumechaguliwa kama vile Mheshimiwa Wachuka husema ya kwamba alipigana na wanaume kumi na wanne na akashinda. Pia sisi tulishinda na kuapishwa hapa, kwa hivyo tupewe heshima.

Bwana Spika, ni aibu sana ya kwamba sisi tulivyochaguliwa na wananchi, kabla mtu apigie daktari au askari, sisi ndio huwa tunapigiwa. Mimi wakati hayo maafa yalitokea, nilipigiwa na wananchi wenzangu lakini sasa sisi hatuna pesa na hiyo ndiyo ukweli. Hatuna pesa zetu kama CDF au NGAF. Wale watu ambao tumeaminia pesa zetu ni hawa mawaziri na naibu wao. Waheshimiwa wakisimama, waongee ukweli. Unapigia mtu simu na kwa sababu yeye aliajiriwa na Gavana, haoni kama sisi tulimpitisha hapa. Watu wanakufa na ukimpigia simu hawezi akachukua Bwana Spika, kwa sababu sisi ni maskini na wanaiba pesa zetu.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

Tutaanza kuwakalisha hapa na taarifa ya kwanza ambayo nitaleta hapa ni ya kwamba kutoka hapa na ieleweke ya kwamba Mheshimiwa Anthony Theuri, Mjumbe ambaye amechaguliwa na watu wa Wadi ya Nanyuki ambaye pia ni naibu wa Spika, hakuna kitu kama *acting*. Kama sheria inasema ni miezi sita, wacha iwe miezi sita kwa sababu hao watu hakuna mahali wanaweza kuajibika. Mtu mwenyewe hauwezi kumuuliza swali na ukimwuliza, anaweka sheria mbele yako. Hivi sasa napiga hesabu na hatuwezi kujua mahali milioni mia moja na arobaini huwa inaenda.

Sasa hivi ukienda katika hii hospitali na ndio huwa inabeba pesa nyingi sana, hakuna madawa. Ikienda kuuliza mtu anasema ya kwamba ako *acting*. Tunataka watu wawajibike. Pesa zetu nyingi zimelala huko na zitarudishwa. Sasa mwaka wa serikali utakuwa unaisha baada ya wiki tatu. Tulikuja hapa na Mheshimiwa Wachuka, Nyokabi, Nicholas na tukaongea na Wabunge wenzetu na kuwaambia ya kwamba watupe pesa ili tutengeneze hospitali kwetu kwa sababu tunaumia na watu wamekuwa wengi. Wakatuonea huruma na kutoa pesa za barabara, maji na shule na kutuambia ziende zikatengeneze hospitali. Ni aibu kubwa kwa sababu sasa hivi tunapoongea hapa hakuna kitu ambacho kimefanywa katika wadi zetu na ninajua ya kwamba Mheshimiwa wachuka akisimama, atasema ni ukweli. Hakuna hospitali na hakuna pesa.

Bwana Spika, kuna shida nyingi katika hii Kenya na tunajua ya kwamba watu wanahitaji pesa. Wakati pesa inawekwa na kurudi huko Nairobi, pesa huwa inapunguzwa na kuonekana ni kama tuliuma ugali kubwa kuliko mdomo yetu. Pesa yetu huwa inapotelea huko. Sasa hivi tunapoongea Bwana Spika na ningeomba uwe makini ili usikie ule uchungu ambao tuko nao, zile Barabara ambazo tumetengeneza juzi, ni aibu kwa sababu ni mwaka wa pili lakini hakuna Mjumbe hapa ambaye amejenga zaidi ya kilomita thelathini. Shida kubwa ni ajira. Kama hatutengenezi Barabara, ajira haitapatikana. Tukipeleka pesa yote hospitali, hao wagonjwa wetu watapelekwa wapi au watapitishwa wapi. Labda tuseme ya kwamba tutatengeneza uwanja wa ndege ili wawe wakipelekwa na *helicopter* kwa sababu hakuna Barabara.

La pili, wale ambao huwa wakienda kazi au shule, watakuwa wakipitia wapi? Mnachukua pesa hapa kwa sababu hili Bunge linaonekana ni kwamba limejigawa. Ninaomba kwa jina la Bwana Yesu hizo mirengo zipate kushindwa na watu warudi laini kwa sababu tunaumizana. Wanachukua pesa na kupelekwa kwa kilimo. Tutaanza kuchunguza hayo mambo yote na kuyaleta hapa. Utakuta ya kwamba Wizara ya Kilimo inapatiwa pesa na kusema ya kwamba watapatiana mbegu Umande, Marmanet au Doldol lakini ukweli wa mambo ni ya kwamba Doldol hakuna mashamba ya kulima. Tunajua ya kwamba pande zingine za Mukogodo Mashariki ni mchanga na Sosian. Watu wameanza kuiba pesa ya serikali wakijificha ilhali wananchi wenzetu wanaumia. Hiyo pesa yote inafaa kupelekwa mahali ambapo itasaidia watu.

Sasa hivi Bwana Spika, utashangaa hiyo hesabu ikiletwa hapa. Kati ya hizo pesa zaidi ya milioni mia moja na arobaini, utakuta ya kwamba nusu ya zile pesa zimetumika. Utapata wakisema ya kwamba walienda Likii wakapeana. Nilikuwa huko na hawakupatiana vitu ambavyo vilipitisha elfu arobaini. Sisi tulipewa pesa na watu wa Msalaba Mwekundu. Tulipatiwa blanketi na godoro. CECM naye na abarikiwe sana, alituletea gunia kadhaa ya mchele na maharagwe. Naomba hili Bunge kwa wakati wa kwanza kwa sababu hatutaishi hapa milele na wale ambao watasaidiwa na Mungu warudi kama mimi, tusimame na watu wetu wakati huu wa hili janga. Hiyo pesa itumiwe vizuri.

Kwangu hakuna Barabara na zilikuwa nzuri. Watu hawaendi shule na wengine wanazunguka shule ya msingi ya Thingithu ambayo nilisomea zaidi ya kilomita nane kwa

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

sababu daraja ilienda na maji. Hadi sasa hiv,i huyo Waziri Nabos kwa sababu hata nilimsahau kwa sababu hawana haja nasi kwa sababu walitutumia kama karatasi ya choo, hautawahi kuona, hakienda kuona hata mara moja. Hata hajui yale madhara ambayo iko.

Bwana Spika, ningeomba kwa mara ya kwanza tuwe makini na hiyo pesa, kazi ifanywe sababu tunaaibika na mvua haijaisha. Kwa hayo mengi ama machache, ninaomba huu mswada uchukuliwe... *(off record)* Naona niko na watu wananiunga mkono na ni vizuri sana. Huu mswada usiwe kama ile miswada ingine za kusukuma. Tuwe makini na hiyo pesa tuitishe, heri igawanywe watu waende hivyo.

Saa hizi, ninasikia Igwamiti kuna watu wamekufa. Juzi nimepigiwa na Mheshimiwa ananiamba yuko mazishi na wengine hawapatikani. Zile barabara ambazo alikua anaringa nazo sasa hakuna, sijui ataambia wananchi namna gani. Saa hizi, kuna magonjwa yamejitokeza ya tumbo na kuhara. Utaenda upate hakuna dawa na pesa ziko huko. Ningeomba hili Bunge tusimame na watu wetu sababu siku moja tutasimama mbele ya Mungu na kila mtu atahukumiwa na zile vitendo ambazo amefanya. Asanteni sana na muunge huu mswada mkono.

Speaker: Thank you, Hon. Anthony Theuri allow me to cross the floor and give the chance to Hon. Wachuka.

Hon. Irene Wachuka: Asante Sana, Bwana Spika. Ningemuuliza Naibu Spika na Hon. Catherine Nyokabi tusikilizane. Kitu ya kwanza nashukuru yule ambaye ameleta huu mjadala. Ya pili, nataka kumwambia mwenye Nyumba ambaye ni Naibu wa Spika arudishe watoto wake kwa laini. Wewe mwenyewe kama Naibu wa Spika tulikushika mkono tukakuleta na wewe ni Baba katika hili Bunge. Uturudishe kwa laini kama sisi watoto tumetoka nje.

Na kila boma ina shida, watoto wanatoka. Sasa ni wakati wako wa kuturudisha laini tujenge hili Bunge. Nimefurahia sana kwa vile nimepata akiongea kuhusu vile ambavyo mambo imeendelea. Kama kuna mtu yuko na uchungu, isipokua ni vile sijamaliza ule uchungu wa mzee, mimi ningepigana na hawa watu wa Gavana. Mmoja akiwa CO ambaye anaitwa Kenneth Kibara na siogopi nikitaja.

Hii sio kwa utaratibu. Mimi nilichaguliwa na watu wa Igwamiti 53,602. Idadi ya watu wa Igwamiti wakaona mimi ninaweza. Nilikuwa nimechaguliwa hapa mara mbili. Mara ya pili tukawa tumechaguliwa tukiwa na Mheshimiwa Catherine Nyokabi tukarudi hapa. Mimi nataka kuongea kinagaubaga. Siogopi hata kama ni vyombo vya habari nitaita. Ukisikia kwamba mimi nimeamua, mimi vita yangu huwa sirudi nyuma.

Liwe liwalo, lazima itapiganwa. Labda Gavana aite watu wake na aite maafisa wake wakuu. Kama hawataki kazi warudishe viti vyetu waende wafanye siasa kwa sababu hatutakubali. Wako mashinani wakifanya siasa badala ya kufanyia watu kazi? Mimi ninaongea kitu hata Gavana akija hapa nitasema. Leo nilimtafuta ikawa yuko na mkutano. Sitaki kutuma mtu, naenda kuonana na yeye ana kwa ana nimwambie kwamba alituletea watu ambao ni wanasiasa. Kazi yao ni siasa.

Unakuta wengine wako Ol-Moran, mwingine anakuja kwangu, saa hii Kenneth Kibara ni yeye Mwakilishi wa Bunge la Kaunti na yeye ndio Ofisa Mkuu. Nataka kujua na kabla sijaambia watu wa Igwamiti tuchukue matawi, wacha mimi nijisaidie. Juzi nilikuwa Kijiji cha Maina. Nyumba ya familia tatu ilichomeka. Nililala huko kutoka saa nane za usiku hadi asubuhi. Wakati tulisema tulete vitu, mimi sikuwa na pesa, nilipeleka godoro kumi na tano kutoka kwa mshahara yangu.

Ilikuwa Ijumaa na siku iliyofuata Waziri wa Mambo ya Utawala kwenye Kaunti akasema ataleta vitu na akaleta Jumamosi. Watu wa Kijiji ya Kiamiana wakamuuliza kwa nini

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

mama yao hakukuja hapa na yeye ndio mwenyeji. Kwa nini hangetaka mimi niende. Alileta vitu za Kaunti blanketi na godoro akasema ni zake. Hii ni kwa utaratibu kweli? Tunapitisha bajeti hapa halafu inakua ya kujenga wanasiasa?

Kwa hivyo, mimi nataka kusema hivi, kama vitu vimetoka katika Kaunti iletwe na isemekane hii ni ya Majanga. Ni kweli ama sio kweli? Kama unataka kuuliza ni sawa tu nitakaa chini tuuulize. Nimekasirika sana. Kama hujaguswa mimi nimeguswa. Wakati kama vile Naibu wa Spika amesema, wananchi hawatauliza Gavana, hatauliza wale, atauliza wewe ambaye ulipewa kura na wananchi.

Ulipewa kura utetee wananchi na sisi hatujashindwa na kazi yetu lakini tumekatwa mikono, tumefungwa miguu. Gavana anawapatia kazi lakini hawafanyi kazi, kazi yao ni siasa huko mashinani. Barabara leo mimi ningetaka kuuliza walio kwenye kiti, Waheshimiwa kumi na tano mketi chini mjue vile barabara zitatengenezwa. Mimi nilikua nimemaliza barabara tatu na zikawa sawa, juzi Mwenyekiti wa Kamati alikuwa kwangu, zote zimeharibika; labda tuanze upya.

Sio kwangu pekee, nafikiria mvua ilinyesha kila wadi ila sio Igwamiti pekee yake. Wadi zote ziko na shida, kila wadi imeguzwa na hili janga la mvua. Kwa hivyo, wakati Naibu wa Spika anaongea, anaongea kitu ambacho kinakera kila mtu ndio maana namwambia arudishe nyumba yake pamoja tukae chini tuongee sisi wote Ishirini na moja tujue jinsi tutaendelea.

Isipokua ni vile sioni Mwenyekiti wa Bajeti, ningetaka nijue katika wadi yangu ya Igwamiti, pesa ambayo tulipeana kwa bajeti ya mwaka uliopita ilifanya nini na nini, nijue ilifanya hii na hii na imebakisha hii. Hii bajeti ingine ninaweka inaenda kufanya nini. Nafikiria pesa nyingi sana ambayo wadi hupewa kwa bajeti ni ya Hospitali kwa sababu kila mtu anakua mgonjwa na hakuna mtu anakuwa na shida wakati anapitisha bajeti ya Hospitali au ya Maji au ya Kilimo.

Ningetaka kujua hata kama umepewa milioni Ishirini kwa Wadi yako, imetumika aje? Sasa, hapa ni giza tu, ni giza tu. Kwa nini Mheshimiwa Irene Wachuka anapopewa pesa, yeye kama CECM anatoroka anaenda kufanya siasa. Naongea kitu ambaye siogopi nikiongea. Sikuchaguliwa niwe nikija kuficha maneno kama yameharibika. Mimi niko hapa kusimama na wakazi wa Igwamiti na nitaendelea kusimama nao kwa sababu ni hao walinileta hapa.

Isipokuwa ni yeye, angefika hapa na singepatana na wajumbe wale wengine. Kwa sababu hatukuja kupiga mtu, sisi tunaongea mambo ambayo yako ndani na Waheshimiwa wako kumi na tano, najua kila Wadi iko na uchungu wake. Tuko wale ambao hatuna mtu wa kutusaidia, kama Mheshimiwa Catherine Nyokabi alitembea pekee yake kila Wadi kuangalia barabara. Kwangu alisema kuna mahali iko na shida na lazima irekebishwe.

Nasimama kuunga mkono na kusema kama bajeti itawekwa irudishe mambo ya barabara na iongezwe juu hakuna barabara. Msiende kusema mtajenga barabara, mtarudi nyumbani nikienda kwa sababu mvua haikukuja kuchagua ila ilifagilia kila kitu. Ikiwa inabeba hadi lami, ni hizi tunajenga na ni mawe tu itabakisha? Nasimama kusema Waheshimiwa wenzangu, tafadhalini tushikane mikono ndio tufanye kazi pamoja.

Tuwe kitu kimoja. Tuwe Muungano. Ndio maana nimesihi Naibu wa Spika, anafaa afanye kazi na watu wake, asiende kusema hapa na pale watu walienda. Wewe ndio ambaye tunakuangalia, sio Spika. Spika ana kazi yake na kazi ya Naibu wake ni kushika watoto wake Ishirini na moja tukae chini pamoja, tuongee pamoja na tujue shida iko wapi. Kama ni sisi tuko na shida, tukae chini tutoe shida tuko nayo tuende pamoja tusimame na serikali hii ya Bunge.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

Bwana Spika tunakueleza sisi tutakuwa kitu kimoja, tutafanya kazi pamoja kutoka leo. Kama mtu anasikia hawezi kufanya kazi na yule, wewe tembea na Yesu na sisi ambao tutabaki, tutabaki tukiendeleza kazi. Asante sana, kwa hayo mengi na machache, asanteni sana wajumbe wenzangu. Ngojeni tusimame na msimamo.

Speaker: Thank you, Hon. Irene Wachuka. Members, I would like to bring to your attention to standing order number 74 and allow me to read it. It says; *'the proceedings to be kept in Kiswahili English or Kenyan Sign Language.'* All proceedings of the assembly shall be conducted in Kiswahili English or Kenyan Sign Language.

To a member who begins a speech in any of the languages provided under paragraph one, shall continue in the same language until the conclusion of that Members speech. I urge the Members, for a long time, this standing order has been contravened. We need to begin our conversations and debates in either of the three Languages. In English from the start to the end, or Kiswahili from start to the end or Sign Language from start to the end.

I would implore the Members, if there is any Member who would wish to use sign language, kindly notify us in advance so that we can procure the services of an interpreter. Thank you so much. As I said, I am going to criss-cross the floor, I want to cross to this other side and give to Hon. Joseph Gitahi.

Hon. Joseph Gitahi: Thank you, Hon. Speaker. I am appreciative because I got this at the right time. I know the Honourable Member has a lot to say and I know that all Members also have a lot to say because they have weighty statements.

Let me say it so that I know they have heavy and weighty statements. Hon. Speaker, I stand to support this motion brought forward by Hon. Stephen Ndiritu regarding the repair of damaged roads and infrastructure across the county. Hon. Speaker, since the rains started, a lot of infrastructure have been damaged whether touching on trade, transport and also in our health centres.

Therefore, it is incumbent upon this government to respond to these issues. Hon. Speaker, as we are speaking the reason you saw I was itching to speak let me support the motion then I will talk about other things later. Roads have been damaged. As we are speaking to you, there is a road that connects at Tandare centre and another one that goes to Miteta, Karumaindo and Kamwenje. This road is very important for security matters. Even though the Members of the County Assembly are not party to the security mechanisms in our areas, we are contributors and stakeholders.

Hon. Speaker, I already made a mistake. This is because the people who are being targeted in our wards are our parents. Hon. Speaker, before they became voters, they were our parents, brothers, sisters, friends and village mates. It is important that we respond to whenever they are in danger. Hon. Speaker, if bandits were to strike today, our people will be vulnerable and they will be left to mercies of these bandits. We do not have urgent response from our security forces because of the nature of the rains that have hit us.

Today if I give you my call logs and messages, I have a lot of complaints in that ward concerning roads that are not able to help security forces to respond to security threats. Additionally, Hon. Speaker, we are a small and fragile economy. Even in our areas we are small and fragile economies that rely on bodaboda and other things. If we cut off trade, we are stifling our people from getting livelihood and food and stuffs and other things. These are issues that we should attend to.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

With regards to issues on budgeting and where the money went to, I support what Hon. Wachuka is saying today that even if we want to support the issues of health centres and infrastructure, I urge Hon. Members that it is good that we listen because we also listened to you. Hon. Speaker, I think we should maintain that discipline so that when one Member is speaking and I am not yelling nonsense here, I am speaking issues.

Hon. Speaker, I am talking about even if we invest in other issues of health and trade, if we leave out roads, then that is logic upside down. So, these issues of budgeting and roads should be taken care of. As I finish Hon. Speaker, while I seated here, I was consuming some statements that are so hypocritical. I am a rebel and I speak my mind on what is in my heart. Some of these Members speaking here are so hypocritical.

As a Member of this County Assembly and as a journalist, I have investigated. Some of these Members took gossip to the Executive to an extent that today, a number of Members of the County Assembly cannot be attended to by Chief Officers and CECM's. I am saying things that I will repeat because tomorrow, I will be in one of the media stations and I am going to repeat exactly this that this Assembly has Members that went to the Executive to take gossip.

Today, I am cut off between the Members of the County Assembly and the Executive. I am wondering which issues are they attending. Do they even understand what is happening in Githiga? When I call a Chief Officer for three consecutive weeks is so that we salvage a situation that is in Githiga yet they cannot pick. I then get an official communication that they were instructed to never to pick calls from some of the Members of the County Assembly.

This is contravention of justice and we will talk about these things even at the top of mountains. Some of these things are so unethical and unprofessional. Some of these people came here and they said that they are very professional. Today, the kind of things that get out of their mouth, it is in such times that it is so difficult to be a Member of the County Assembly. I have all the complaints and the grievances from my ward.

Yesterday, another Chief Officer as late as yesterday lies to me that they are not in the office only to find them in a bar with some of the Members of the County Assembly here. Such things are so shameful when some people are now claiming here that some Chief Officers are roaming all over their wards. It is them who told these Chief Officers that sometimes not to pick calls from so and so. There is no problem because people can see because they are not fools.

Hon. Speaker, I want to make this statement that you can silence somebody but it doesn't mean you have converted them. You can contravene all their rights but we will be there to fight on. On that matter, we will listen to reggae. There is a musician called Bob Marley and as he finishes his redemption song, he says that *"I am not afraid of any atomic energy, none of them are going to stop the times."*

It is important that we get sober. It is also important that we get clear on the matters that we are saying. Hon. Speaker, you cannot speak from both sides of the mouth. Today you come and speak this and tomorrow you speak the other thing. We are watching and you know the history of this context, some of us have nothing else to lose. We are no longer chairpersons but we will continue asking from accountability from this government from morning to evening and we will not count.

These are the things I am going to speak from now, to the media and other entities so that this County gets back. Mr. Speaker, how do we explain that today, I will have an issue with hospitals. The Chief Officer has decided not to work and some of them, I want to say

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

without avoidance even working with former competitors; I am asking what is happening to this county.

Some of them have lied to H.E the Governor to an extent that to date, we do not have ward administrators. Fortunately, Hon. Wachuka had an emergency at her ward and she was attended to. Mine has never been attended to. People had an inferno. They will not attend to my ward but they will attend Wachuka's because of the context of this matter. The citizen can see and it is good to speak people's heart.

Mr. Speaker, the reason as to why you do not see me mostly in these Assembly is because I am in the ground attending to these people. Even if the Chief Officer or the CECM will not pick, I will be there with these people because it is their sentiment that due to the ignorance of some people here, to me this Assembly session is already lost. I am on the ground praying that I come for another one term here.

Next time when we come here, we will not repeat some of the grievous mistakes that have been repeated here to the extent there is no difference between a commoner and a Member of the County Assembly. So, Hon. Speaker, before the issues get so hot, I support this motion that we have repairs. In the Bible, I do not know where but if the Deputy Speaker was here, he would have reminded me which verse but there is somewhere in the Bible that says there is somebody who spoke to a rock and said even if you do not respond, I have already said and you have heard.

